

**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO**  
**ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL (S. 3874)**  
**P.O.Box 6083 – Morogoro**  
Tel. 0689-783630 (Ofisi Taaluma)  
0689-783672 (Bweni la kike) / 0689-782670 (Bweni la kiume)  
0789-978886 (Airtel Money)  
www.alfashule.ac.tz

**TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO**

Ndugu ....., tunafurahi kukujulisha umepata nafasi ya kujiunga na kidato cha tano kwenye shule yetu iliyoko katika manispa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

Ada ni:

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 600,000 kwa mwaka.
  - (b) Kwa mwanafunzi wa bweni Tsh. 1,100,000 kwa mwaka.
- Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 150,000 (kutwa) au 275,000 (bweni) kabla ya kila nusu mhula, lakini bila robo hiyo hutapokewa.

Kwa usalama wa wote unaombwa ulipie benki (akaunti yenye jina la shule iko MKOMBOZI C.B. ikiwa na namba 00120603517801; iko pia CRDB, namba 01J2077746000) halafu vocha uilete shuleni.

Shule imekubaliwa pia kuwa wakala wa kampuni ya simu kwa ajili ya kutuma pesa kwa urahisi zaidi. Namba ya Airtel Money ni 0789-978886 na inatumika kwa mawasiliano na kwa kutuma pesa.

Bila ya kutimiza malipo yote yanayotakiwa hutapokewa.

Ukichelewa kuleta ofisini mwetu vocha ya benki nafasi yako anaweza akapewa mwingine.

Masomo yataanza tarehe 20-7-2020 au siku yoyote baada ya hapo serikali itakaporuhusu. Basi:

(a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufike shuleni tarehe hiyo saa 1:15 asubuhi. Ukichelewa wiki moja kuripoti na kuleta vocha ya benki nafasi yako anaweza akapewa mwingine.

(b) Ukitaka kukaa bweni ufike kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa waliowahi kuleta vocha ya benki hata kabla ya tarehe hiyo).

Ulete vifuatavyo pia:

1. Sare kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyingine):

(a) Kwa wasichana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 25 kutoka ardhini)
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, tracksuit ya buluu na raba
- (vii) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika
- (viii) Waislamu, kwa ombi la mzazi/mlezi, wanaweza wakaruhusiwa kuvaa hijabu halisi nyeupe isiyo na pambo mradi wanyoe nywele zote

(b) Kwa wavulana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika.

2. Kwa kukaa bweni:

- (a) Fulana ya kijani yenye maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka ya rangi ya pinki au buluu bahari na blanketi
- (d) Chandarua iliyotiwa dawa
- (e) Godoro jipya la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Taulo na vifaa vingine vya usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote.

N.B. Mashati, fulana, sketi, suruali na sweta ni lazima vinunuliwe shuleni. Pia madaftari, kalamu na vifaa vya hisabati vinapatikana shuleni kwa bei nafuu. Wanafunzi wa somo la Hisabati wasikose kuleta "scientific calculator" na wale wa Biolojia "dissection kit".

